JUA
GAZETI LA MAENDELEO
Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 441

# Raïa wazulumiwa

## Askari kapinga Askofu Monsengwo

Tangu mizozo ya kisiasa kuzuka nchini kati ya vikundi viwili: Kundi lamuunga mkono Raïs wa jamhuri na lile lategemea upinzani na siasa kali tuseme kwa kifupi makundi ya mabwana Mobutu na Tshisekedi, raïa wazulumiwa kutokana na ukosefu wa usalama wa wakaaji na mali zao. Hali hiyo ikiwatia wote uwasiwasi yazungumuziwa mijini na vijijini kote. Wote wanaogandamizwa wajiuliza jawabu litatoka wapi. Ni karibu kila siku watu wawauwa bure, wanyanganywa mali zao, vifaa huibwa ama huunguzwa, nyumba huvunjwa ama huchomwa ovyo ovyo ni hasa mjini mkuu Kinshasa. Pia samani ya pesa hupunguka kwa mwendo wa mporomoko wa maji na bei ya vyakula na vifaa kazaa hupandishwa ginsi mchuuzi apenda kwa mwendo wa kunguru. Na hiyo siku nenda rudi. Kwa mshangao mkubwa watenda maovu ao wanaowasukuma hawagunduliwi. Kwa kweli tunayo haki ya kujiuliza kama viongozi, wote wanaohusika na usalama pia askari walinda amani kazi gani wafanya.

Serkali ya mpito na wengineo viongozi nchini wanao madaraka ya kustarehesha amani na usalama nchini na mipakani. Mikutano ya masikilizano kati ya wanasiasa huendeshwa kwa kufikilia njia bora ya kusimika na kustarehesha amani. Na siyo mzaa. Ni tatizo kubwa kweli. Lakini mipango gani kachukuliwa kwa jambo hilo mbele ya kupata jawabu kweli? Hata askari jeshi wamoja kaombwa kurudi kampini ingawa wangali bado na kazi nyingi zakufanya.

Basi mpaka wakati gani magumu ambayo yaangamiza raïa yatakwisha ? Ni ulizo larudia kila mara midomoni mwa watu. Jibu litatoka tu kwenyi viongozi wa nchi, mabingwa wa siasa ambao wagongana na askari jeshi.Twajua wote kuwa wamebadili kiongozi mkuu wa majeshi ya askari. Jemadari Mahele kagombolewa na jemadari Eluki. Na huyu kawakusanya maakida wakuu wa viongozi wakuu wa vikosi vya askari jeshi. Twazani kama hatua kazaa wa kazaa kachukuliwa kwa kutia usawa katika majeshi. Lakini yaonekana kuwa hakuna hata mabadiliko mamoja yatezamiwa kuweko.

Viongozi wakuu nchini watanena kuwa hakika kajitahidi kwa juhudi kubwa kustarehesha usalama wa watu na mali zao. Ingawa raïa waendelea kuangamizwa na kutangatanga mahali mengi kama vile wakimbizi wa kisiasa nchini mwao. Aweza tu kudanganyiwa mtu ambaye atajiachilia kudangaywa kama hao marugaruga wa kufiatua risasi, kutumia silaha kazaa za kisasa, kuiba, kuchoma nyumba na viwanda na kutenda mengineo maovu wataendelea kuwazulumu wakaaji na raïa. Askari jeshi wapaswa kutumika nguvu zaidi, kuonya nia yao bora na zamiri za kazi yao ili wasizaniwe kuwa ndio kweli msinji wa misukosuko, fujo na hali ya vitisho yapatikana nchini. Kutokana na vitendo vyao na shuhudi zatolewa.

### Vitendo vya ujeuri

Baada ya vitendo vya ujeuri kaendeshwa na askari-jeshi hapo majuzi tangu tarehe 24 hadi 27 Februari 1993 mjini Kinshasa, askofu Monsengwo Pasinya, prezidenti wa Baraza kuu la washauri wa Jamhuri katoa maoni yake kuhusu jambo hilo la hofu. Kwa kuwa askari hao, wake na watoto wao kwa amri ya viongozi wakuu wa vikosi vya askari kawateka nyara washauri wa Jamhuri muda wa siku tatu na makao ya Askofu Monsengwo pia. Hawa wakiwa na nia mbya ya kumuua, kasemwa huko.

Kwa kweli vitendo kaesha askari-jeshi na masemi ya jemadari Eluki, kiongozi mpya wa makao (ofisi) makuu ya vikosi vya askari-jeshi, katia uwasiwasi nchini. Kwani Jemadari Eluki kamshtumu Askofu Monsengwo kuwa ndiye mshinji wa misukosuko, chuki, ujeuri na ubaguzi wa kabila nchini pahali pa kuwa muunganishi wa raïa. Toka hayo, askari-jeshi, kwa kinywa cha jemadari huyo, eti hawatambuwe viungo kasimikwa na Mkutano mkuu wa kitaifa bali tu, mpaka sasa, Mareshali Mobutu kama vile raisi wa Jamhuri na mwakilishi pekee wa raïa wa Zaïre, kiongozi mkuu na mkamilifu wa Taifa na wa viosi vya askari. Na toka hiyo, wa mpinga Askofu Monsengwo, mwenyikiti wa Baraza kuu la washauri wa Jamhuri.

Kwa ngambo yake Askofu Monsengwo atupilia mbali mashitaka hayo na aomba mbele ya Mkutano wa masikilizano kati ya Rais Mubutu, Askofu Monsengwo, Waziri mkuu Tshisekedi na wawakilishi yapata makumi matatu wa vikundi vikuu kumi na tano vya kisiasa yafaa kwanza Raïs Mobutu atowe mwanga kamili kuhusu vitendo hivyo vya uzulumu na waliotoa amri viendeshwe na kupewa azabu. Raïs Mobutu akajibu kwa maoni hayo, asisitiza mkutano huo kafanyike kwa kuondoa nchi katika shimo ilimo na kutafuta jawabu kwa mzozo wa kisiasa ulio kwa sasa nchini. Na toka hapo viungo vya mpito kasimikwa na mkutano mkuu vipate kutumika ginsi kahitajika kidemokrasia na mambo ya ombwa yataweza kuchunguliwa kwa karibu na kupata majawabu.

Bwana Tshisekedi, yeye anena kuwa yupo tayari kushiriki kwenyi mkutano huo muhimu kama kweli ni kwa manufaa ya raïa. Hata ikiwa utaendeshwa chumbani mwa kulala cha Raïs Mobutu. Bwana Tshisekedi atahuzuria mkutano huo kama oroza ya mkutano utatolewa mbele ya wakati ili kuelewa vema yatakayotatuliwa na kutoa majibu bora kwa mambo yatakayoulizwa kwa kuepuka kujibu ovyo ovyo na majawabu ya kweli na ya kudumu yapatikane.

Kuhusu pia hali ya kisiasa iliyoko, hasa ngambo ya upinzani mkali, imejulishwa kuwa mmoja kati ya wapinzani wakuu, Bwana Faustino Birindwa, wa chama cha kisiasa "UDPS", kafukuzwa chamani kutokana, wasemavyo viongozi wa chama hicho, na mwenendo wake usio halali. Kwani hakuwa tena na msimamo kamili katika siasa kahitajika na chama "UDPS". Kwa kuwa alianza kuenda kinyume cha kanuni na hatua zachukuliwa na kamati kuu kiongozi cha chama hicho.

**André Bisimwa L-B. Tserou**

## UHARIRI

# Shangwe na shukrani

Kutokana na hali ya kisiasa, ya kijamii na ya kiuchumi iliyo nchini, uwasiwasi wawashika raïa na maisha huwa ngumu siku kwa siku. Hasa kutokana na kupandishwa kwa bei ya vyakula na vinginevyo vifaa kwa jumla na jimboni mwa Kivu ya Kusini kwa upekee hasa mjini Bukavu imeonekana kuwa siku zijazo hali nenda kawa mbovu zaidi. Na hiyo, kama shirika la wafanyabiashara nchini Zaire ama "ANEZA" halikuchukua mipango kazaa yatezamiwa kweli bora kwa kurekebisha bei ya bizaa. Kwani toka viongozi wamoja nchini kukazania noti za milioni tano zitumiwe na ambazo hazikubaliwe madukani kama vile sokoni, maandamano, hasara na mauaji mengi katukia. Na viongozi hao wasijue vinyume haramu katukia wakiona faida zao wenyewe. Bali pia wafanyabiashara wataka kuwinia miongoni mwa wenzio. Kwa kuwa hawa wapandisha bei vile wataka wakizarau sheria na atuwa za serkali. Nia ya wafanyabiashara wanao zamiri ya maendeleo na ya huruma kwa kufikilia kurahisisha maisha ya raïa ni ya kusifiwa na kila mtu ahusikiwa.

Kweli utashi bora wa wafanyabiashara kwa kustarehesha amani, usalama wa watu na mali zao na toka hayo urahisi wa maisha kaonywa. Utahidi kafanywa na wafanyabiashara hao pia mashirika kazaa ambao kakusanya kiasi kikubwa cha feza kwa kulipa mishahara ya askari-jeshi hapo majuzi ni wa kupigiliwa shangwe na vigelegele. Kwa kuwa feza katumwa na viongozi mjini Kinshasa zilikuwa hizo za noti ya milloni tano ambayo kapigwa marufuku na serkali ya mpito kaongozwa na bwana Tshisekedi na kukataliwa matumizi mahali mengi nchini. Pia utashi wa mchuuzi mkuu moja mjini Bukavu wa kubadili dolari moja ya kiamerikani kwa zaire 2.800.000 Z uliwatikisa wenzie. Kwa kuwa samani ya dolari kapunguka. Na toka kitendo hicho, wachuuzi wengine katishwa kwa kuwa walikuwa wakiwaangamiza wakaaji wakitunga zao bei zisizolingana na hizo kasimikwa na serkali wakilinganisha bei ya vitu na samani ya dolari ingawa pato ao mshahara wa wanunuzi hailinganishwi na samani ya feza hizo za kigeni. Bali pia watu hawapokee mishahara yao ama hawaipate kwa wakati ao kama inavyofaa. Toka kitendo hicho cha mfanyabiashara huyo, wengine kafuata mfano wake. Na bila kusita bei ya mafuta ya gari, "esansi na mazutu" kashushwa na hapo tarifa ya usafirishaji wa watu na vifaa vyao kaonekana yenyi kubadili. Kwani, kwa mfano, kitambo kimoja kwa taxi chalipwa sasa zaire 500.000. Silo jambo hilo tu bali pia baada ya kukutana na wawakilishi wa wafanyabiashara kupitia shirika lao "Aneza", liwali wa jimbo la Kivu ya Kusini, mchungaji Kyembwa, kachukuwa hatua mihimu. Kati ya hatua hizo, imelazimishwa kwa wafanyabiashara na mashirika kutoa ushuru wao kwa vyumba vya serkali vinavyohusika kwa kiasi cha feza kamili na kingine kwa njia ya hawala (chèque) kwa kutimiza mapaswa yao na kujaza hivi sanduku la serkali kwenyi Benki kuu jimboni na toka hapo kupatikane jawabu kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa serkali na wengineo. Kwa kuwa kutokana na ukosefu wa feza kunako mabenki, magumu mengi kawakumba wakaaji.

Basi, kumbe ni wafanyabiashara walio na nia mbaya ya kuwinia miongoni mwa wenzio raïa ndio wakukwamisha urahisi wa maisha wakitimua wakaaji kwa magendo. Na kutaka hivi kuwaangamiza wakijua kweli kuwa pato la ndugu zao haliwezi kamwe kulinganishwa na mahitaji yao. Ni toka nguvu yafanywa na hatua kachukuliwa na shirika "Aneza", kuungwa mkono na Shirika la kiraïa ama "Société civile" na wengineo wanaohusika, ndiyo yatezamiwa kuwa raïa na wengineo wakaaji watapumua siku zijazo. Ouf ! Shangwe na shukrani kwao.

**Na André Bisimwa L-B. Tserou**

Tuzungumze :

# Gani habari ya kweli ?

Baada ya mamlaka tatu ya serkali : mamlaka ya kutenda (pouvoir exécutif), mamlaka ya sheria (pouvoir législatif) na mamlaka ya haki (pouvoir judiciaire), kuna mamlaka ya kupasha habari (pouvoir d'informer) iitwayo mamlaka ya ine. Makundi ya watu hayawezi kuishi bila kupasha habari kwa wengine. Lazima hiyo kaonekana tangu awali. Popote tukaapo na tuendapo tunayo lazima ya kuelewana na wengine. Ila katika upashaji wa habari kuna mipaka fulani fulani. Ndio sababu twakuta watu wa aina mbalimbali wakisumulia kuhusu kundi lao binafsi na mengineo.

Hata ikiwa mtu azungumza na mwengine kwa jambo fulani, huyo si mpasha-habari ila msemaji tu. Siku hizi mambo yapinduka na watu husikia mengi na kusema mengi isiyo na maana. Karibu idadi kubwa wazungumzia mambo ya siasa kadiri watumwa na mafikiri yao bila kujulisha wapi watosha habari mbalimbali. Wengi usema uwongo na kusingizia mara na mara eti wamesikia habari kutoka redio ya Ufransa ao ya Ujerumani ya magaribi ijapo kuwa ni mambo yatoka kichwani mwao binafsi. Ndio sababu taifa kupitia raia lachanganikiwa, la lewa-lewa kwa habari nyingi na halijui lifuate habari gani iliyo kweli.

Ingelikuwa vema, raia wafuate habari zatolewa na wanahabari (journalistes) na viongozi wengine kazaa wanaoaminika kutoa habari kwa kweli bila upendeleo ao faida yoyote. Ni kama vile viongozi wa dini, wakuu wa shirika la kiraia. Katika kupasha habari inafaa kutopendelea upande wowote. Hivyo utajua ukweli walala wapi. Na kwa kujua ukweli huo mtu astahili kuchungua mambo na kuelewa. Kwa kuwa habari ya kweli na yenyi kuaminika, ni lazima habari hiyo kutimiza mashurti yafuatayo : Kwanza kujua nani asemae, asema nini, kwa nani, kwa njia gani na kuna tukio [illegible]?

Bila hayo, habari yoyote yaingia mashakani na haiaminiki hata kidogo. Na hapo yaweza kuonekana uwongo mtupu. Tukumbukeni maneno kaimba Lwambo Franco : "Mwongo na mlozi ni watu wakuchoma". Sasa siku za leo twaona hata watu wenyi elimu pia hutumikisha uwongo kama silaha ya kujitetea. Tabia kama ile yaweza kuwapeleka watu gorogoroni. Mtu aheshimika kwa maneno azungumzayo. Na mwanamziki mwengine kasema "Mbele yakutoa habari chunguza, fanya upelelezi wa kujua ukweli upi" (Vérifiez, sala nano enquête). Rekebisha ulimi wako. Kwani mambo wasema hayarudi na yamesikilika.

**Mutungwa abandelwa Phély**